TANGAZO LA SERIKALI Na. 153 la tarehe 14/3/2025

SHERIA YA FIDIA KWA WAFANYAKAZI,
(SURA 263)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 94)*

KANUNI ZA FIDIA KWA WAFANYAKAZI ( FAO LA UTENGAMAO) ZA MWAKA 2025

## MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Jina*

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.
4. Utoaji wa fao la utengamao.

SHERIA YA FIDIA KWA WAFANYAKAZI,
(SURA 263)

## KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 94)*

KANUNI ZA FIDIA KWA WAFANYAKAZI (FAO LA UTENGAMAO) ZA MWAKA 2025

KWA KUWA, chini ya kifungu cha 69 cha Sheria, Mkurugenzi Mkuu amepewa mamlaka ya kutoa fao la utengamao kwa wafanyakazi ambao wamepata madhara kutokana na ajali au magonjwa yanayotokana na kazi;

KWA KUWA, kwa mujibu wa Kanuni za Fidia kwa Wafanyakazi za Mwaka 2016 malipo ya faida ya utengamao yataanzishwa baada ya Waziri kutoa kanuni maalumu kwa ajili hiyo;

NA KWA KUWA, kwa kuzingatia kifungu cha 94(h) cha Sheria, Waziri anaweza kutengeneza kanuni kuainisha suala lolote ili kutekeleza masharti ya Sheria;

HIVYO BASI, Mimi, RIDHIWANI J. KIKWETE, natengeneza Kanuni hizi kwa madhumuni ya kutekeleza fao la utengamao ambalo linaweza kutolewa na Mkurugenzi Mkuu kwa mfanyakazi yeyote ambaye amepata madhara kutokana na ajali au magonjwa yanayotokana na kazi.

Jina

**1**. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Fidia kwa Wafanyakazi (Fao la Utengamao) za Mwaka 2025.

Matumizi

**2**. Kanuni hizi zitatumika kwa wafanyakazi wote Tanzania Bara.

Tafsiri

**3**. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitajika vinginevyo-

"fao la utengamao" maana yake ni huduma za utengamao wa kijamii na ufundi zinazotolewa kwa mfanyakazi

mwenye ulemavu wa kudumu unaotokana na ajali au magonjwa yanayotokana na kazi kwa mujibu wa kifungu cha 69 cha Sheria;

"utengamao" maana yake ni juhudi za pamoja katika nyanja za afya, elimu, saikolojia na kazi, ambazo zinakusudiwa kuinua kiwango cha kazi cha mfanyakazi ambaye amepata ulemavu wa kudumu unaotokana na ajali au ugonjwa unaotokana na kazi ili kumwezesha kushiriki katika maisha ya kawaida katika jamii;

"Mwongozo wa Fao la Utengamao" maana yake ni mwongozo wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi uliotolewa na Mkurugenzi Mkuu; na

Sura ya 263 "Sheria" maana yake ni Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi.

Utoaji wa fao la utengamao Sura ya 263

**4.**-(1) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 69 cha Sheria, mfanyakazi anaweza kuomba fao la utengamao katika namna itakavyoainishwa katika Mwongozo wa Fao la Utengamao.

(2) Bila kujali kanuni ndogo ya (1), iwapo kwa maoni ya Mkurugenzi Mkuu mfanyakazi ambaye amepata majeraha kutokana na ajali mahali pa kazi au ugonjwa. unaotokana na kazi anahitaji huduma za utengamao anaweza kwa idhini ya mfanyakazi kutoa fao la utengamao kwa mfanyakazi huyo.

Dodoma,
4 Mchi, 2025

RIDHIWANI J. KIKWETE,
*Waziri wa Nchi*, *Ofisi ya Waziri Mkuu*, *Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu*